OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

MKOA WA RUVUMA
SIMU: 0689241186/0763021890

SHULE YA SEKONDARI LUKUMBULE
S. L. P 322,
TUNDURU.

Kumb.Na.LSS/E.6/12/VOL.1/08 14/12/2020

Ndugu …….

S/M …….

TUNDURU.

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari LUKUMBULE mwaka 2020.

Aidha natumia nafasi hii kukupongeza kwa kufaulu vizuri mtihani wako wa kumaliza Elimu ya Msingi. Mafanikio hayo yamekufanya uchaguliwe kuendelea na masomo ya sekondari. Wenzako wengi uliomaliza nao hawakupata nafasi hii adimu. Hivyo ni matumaini yangu kuwa utaitumia nafasi hii kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

Shule ya Sekondari Lukumbule ipo katika kijiji cha Mchesi, Kata ya Mchesi, Tarafa ya Lukumbule kilometa 66 kusini mwa mji wa Tunduru. Unapowasili Kijijini kutokea mji wa Tunduru, kibao kitakuonyesha shule ilipo. Kila mwanafunzi atajitegemea kwa safari zote za kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo au kwa dharula yoyote ile.

Shule hii ni ya kutwa, ila ina hosteli (nyumba za kulala) kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka vijiji vya mbali. Mwanafunzi atakayekaa hosteli ni lazima aje na vifaa vya kulalia na chakula kwa mujibu wa maelekezo.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo:-

1. Fomu ya Maelekezo ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020.
2. Fomu ya kupimwa Afya na Mganga Mkuu katika hospitali ya mkoa, wilaya au kituo cha afya.
3. Fomu ya kuandikishwa shuleni na Taarifa za mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu hizo zote kwa ukamilifu na kuzirejesha hapa shuleni siku ya kuripoti. Mwanafunzi **HATAPOKELEWA** shuleni endapo atakuwa hajakamilisha taratibu zilizoelekezwa. **Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 06/01/2020** na masomo yataanza mara tu baada ya kusajiliwa siku hiyo. Mwanafunzi atakayechelewa wiki mbili tangu tarehe ya kuripoti ,mzazi wake atashitakiwa polisi na baadae mahakamani.

Nakutakia safari njema ya kuja hapa shuleni.

……
SOLOMON REMIGIUS KOMBA
MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI LUKUMBULE.

MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA …….

Ndugu ……
S/M …….
TUNDURU.

1. Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020, na unatakiwa kuripoti siku hiyo ya ufunguzi.
2. Unatakiwa kuripoti shuleni ukiwa na mahitaji yafuatayo:-

1.2 SARE ZA SHULE

WAVULANA

(i) Suruali mbili (2) kitambaa cha rangi ya kijivu mpauko zilizoshonwa kiheshima ndefu (zisibane makalio wala miguu (model).
(ii) Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi (aina ya Tomato).
(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vinavyofungwa kwa gidamu/kamba.
(iv) Soksi nyeupe jozi mbili (2)
(v) Jezi nyekundu (simba), viatu aina ya raba na soksi kwa ajili ya michezo.
(vi) Suruali nyeusi mbili (2) na T-shirt ya rangi ya njano (babalansi) kwa ajili ya kazi.
(vii) Shuka mbili (2) za rangi ya bluu.

NB: Sare itakayonunuliwa au kushonwa kinyume na maelekezo haitakubaliwa.

WASICHANA

(i) Sketi mbili (2) kitambaa cha rangi ya kijivu mpauko. Ziwe ndefu zinazovuka magoti na zenye marinda, (zishonwe kiheshima).
(ii) Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi (aina ya Tomato).
(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vinavyofungwa kwa gidamu/kamba.
(iv) Soksi nyeupe jozi mbili (2).
(v) Track Suit ya rangi ya njano, viatu aina ya raba na soksi kwa ajili ya michezo.
(vi) Sketi mbili (2) rangi nyeusi na T-shirt ya rangi ya bluu (babalansi) kwa ajili ya kazi.
(vii) Shuka mbili (2) za rangi ya pink.

NB: Wanaotaka kushona sare ya HIJABU washone suruali ya kitambaa cha sketi kilichotajwa. Sare itakayoshonwa kinyume na maelekezo haitakubaliwa.

3.2 VIFAA VYA KAZI

Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:-
(i)Jembe moja (1) jipya (Ngwamba) lenye mpini. Jembe chakavu lililotumika halitapokelewa.
(ii)Panga moja (1) jipya.
(iii)Fyagio wa ndani wa dukani wenye mpini mrefu mmoja (1) na wa chelewa mmoja (1).
(iv)Ndoo ndogo mbili (2) za kuchotea maji za lita 10 kila moja.

4.2 VIFAA VYA DARASANI

(i) Daftari kubwa 15, kalamu za kuandikia (peni na penseli na kifutio)
(ii) Mfuko wa kubebea madaftari (school bag)
(iii) Mkebe (mathematical set) na rula ndefu ya futi moja au cm 30.

MAAGIZO KWA WANAFUNZI WATAKAOKAA HOSTELI ZA SHULE

1.3 VIFAA VYA KULALIA

(i) Godoro moja lenye ukubwa wa futi 2 na nusu kwa 6 na kitanda chake.
(ii) Shuka mbili (2) rangi ya bluu kwa wavulana, rangi ya pink kwa wasichana na blanket moja.
(iii) Chandarua kimoja (1).
(iv) Mto wa kulalia wenye foronya ya rangi ya pink kwa wasichana na bluu kwa wavulana.

2.3 MAHITAJI YA CHAKULA

(i) Mahindi kilo 74 kwa muhula au 148 kwa mwaka.
(ii) Maharage au kunde kilo 30 kwa muhula au 60 kwa mwaka.
(iii) Mafuta ya kupikia lita 3 kwa muhula au lita 6 kwa mwaka.
(iv) Chumvi kilo 5 kwa muhula au 10 kwa mwaka.
(v) Fedha ya kusaga nafaka na Posho ya mpishi Tsh. 10,000/= au Tsh. 20,000/= kwa mwaka.

NB: Wanafunzi wa kutwa watachangia fedha ya kusaga na mpishi Tsh 12,500/= kwa mwaka.

3.3 MAHITAJI MENGINE

(i) Cheti cha daktari kuthibitisha afya yako. Fomu imeambatanishwa.
(ii) Cheti cha kuzaliwa au hati ya uraia.
(iii) Jaza fomu ya kuandikishwa shuleni na Taarifa za mzazi/mlezi wa mwanafunzi. Fomu imeambatanishwa.

Nakukaribisha **LUKUMBULE SEKONDARI**, uwe na mwanzo mzuri wa kujenga maisha yako, jamii na Taifa lako.

Ahsante.

TAHADHARI: MWANAFUNZI AMBAYE HATAKAMILISHA MAHITAJI TAJWA HATAPOKELEWA.

SHULE YA SEKONDARI LUKUMBULE

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI (KAMA LILIVYOTUMIKA KWENYE MTIHANI WA DARASA LA VII)
   ……
2. MAHALI NA WILAYA ULIPOZALIWA …….
   DINI ……..DHEHEBU ……KABILA ……..
3. TAREHE YA KUZALIWA ……..
4. SHULE ULIYOHITIMU DARASA LA SABA ……
5. KIDATO UNACHOKUJA KUJIUNGA HAPA SHULE ……
6. JINA LA BABA……HAI/AMEKUFA ……
7. JINA LA MAMA ……HAI/AMEKUFA ……
8. JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HUNA MZAZI) ……
9. UHUSIANO NA MLEZI …….
10. KAZI YA MZAZI /MLEZI ……
    (MKULIMA, MWALIMU, ASKARI POLISI, MFANYABIASHARA, MCHUNGAJI/SHEKHE)
11. KAMA NI MKULIMA, ZAO LA MUHIMU ANALOLITEGEMEA ……
12. KAMA NI MFANYAKAZI, KAZI YAKE NI ……..
13. KAMA NI MFANYABIASHARA, BIASHARA YAKE NI ……..
14. ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……..
15. **JAMAA KATIKA FAMILIA** :-
    (a) IDADI YA WATOTO WA KIUME …….
    (b) IDADI YA WATOTO WA KIKE ……..
    (c) WEWE NI WA NGAPI KATIKA FAMILIA HIYO ……..

16. SHULE ULIZOWAHI KUSOMA :-

SHULE	WILAYA	DARASA	MWAKA

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

MKOA WA RUVUMA
SIMU: 0689241186/0763021890

SHULE YA SEKONDARI LUKUMBULE
S. L. P 322,
TUNDURU.

DATE……

THE MEDICAL OFFICER

……

PUPILS FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by the medical officer.

1. Pupils full name……..
2. Age (years)……Sex……..
3. Blood group and count (Red and white)……
4. Stool examination……..
5. Urinalysis……..
6. Syphilis……..
7. Venereal diseases……..
8. T.B examination ……
9. Eye examination ……..
10. Ear examination ……..
11. Chest examination ……
12. Spleen examination……..
13. Abdominal examination……..
14. Urine for plan test……..

ADDITIONAL INFORMATION/COMMENT (If any) e.g. physical defects or impairment (s) arm, leg, infections, chronic or family diseases etc

……
……
……
……

I certify the above pupil to pursue with his/her education as per the examination conducted above.

Designation……..

Station……..

Signature……Date……..